Caritas

Caritas ni mtandao wa mashirika ya misaada ya Kanisa Katoliki duniani, unaojumuisha mashirika zaidi ya 160 kutoka nchi mbalimbali Kimataifa yaani (**Caritas Internationalis).** Katika kila nchi au jimbo, jina huitwa kutokana na eneo mahalia, mfano; "Caritas Tanzania," "Caritas Kenya," au "Caritas Dar es Salaam". "Caritas" ni neno la linatokana na lugha ya Kilatini likimaanisha **upendo wa huruma**

Caritas Tanzania kama **idara ya maendeleo ya kijamii na misaada ya Kanisa Katoliki Tanzania**, inayofanya kazi chini ya Tanzania Episcopal Conference (TEC). Ilianzishwa mwaka 1971 ili kuratibu shughuli za maendeleo na misaada katika majimbo yote ya Kanisa Katoliki nchini.

Kazi zake kuu ni:

- **Kuratibu maendeleo ya jamii** – Hushirikiana na majimbo ya Kanisa kuandaa na kusimamia miradi ya maendeleo kama kilimo, maji, elimu, afya na kujenga uwezo wa wananchi kujitegemea.
- **Kutoa misaada ya kibinadamu** – Hutoa msaada wakati wa majanga kama mafuriko, ukame, njaa na dharura nyingine, pamoja na kusaidia jamii kujiandaa kukabiliana na majanga.
- **Kukuza haki za binadamu na usawa wa kijinsia** – Huendesha programu zinazohamasisha usawa wa kijinsia, haki za binadamu na ushiriki wa wananchi katika maendeleo.
- **Kushauri na kujenga uwezo wa majimbo** – Hutoa mafunzo, ushauri wa kitaalamu na kusaidia majimbo kuandaa na kusimamia miradi ya maendeleo kwa ufanisi.
- **Utetezi wa masuala ya maendeleo** – Hushiriki katika mijadala na utetezi kuhusu masuala ya maendeleo, ustawi wa jamii na sera zinazogusa maisha ya wananchi.

Kwa upande wa muundo wa kazi, Caritas Tanzania hufanya kazi kama **ofisi ya kitaifa**, huku kila jimbo Katoliki likiwa na ofisi yake ya Caritas inayotekeleza miradi katika eneo lake. Ofisi ya kitaifa huratibu, kutoa mwongozo, kutafuta rasilimali na kuhakikisha majimbo yanashirikiana vizuri

Malengo ya Caritas ni kuendeleza:

- Uinjilishaji wa matendo Huruma na upendo wa Kikristo kwa vitendo**.**
- Misaada ya kibinadamu kwa walioathirika na majanga kama vile mafuriko, ukame, vita au magonjwa.
- Maendeleo endelevu ya jamii, hasa katika maeneo masikini au yaliyo katika hatari.

- Haki za binadamu na ustawi wa jamii, ikiwemo kulinda mazingira na kupinga ukosefu wa usawa.

Caritas Jimbo Kuu la Dar es Salaam

Uwepo wa Shirika hili unaangaziwa tokea Mwaka 1972 na kuimarika zaidi kuanzia 1978. Shirika linafanya shughuli zake katika Wilaya Saba zilizoko ukanda wa Pwani ya Dar es Salaam ikihusisha; Kibaha, Kisarawe, Rufiji, Mkuranga, Mafia, Temeke, Ilala na Kinondoni.

Baada ya kuundwa kwakwe, Caritasi DSM imekuwa na Mikakati mbalimbali ya kushughulikia changamoto za kimaendeleo Dar es Salaam na Pwani; Kupunguza umaskini, Kuwainua Wanawake, Kilimo endelevu, Haki za Binadamu, Madawa ya kulevya na utunzaji wa Mazingira, Afya na uwezeshaji wa jimii kiuchumi**.**

Pia, Caritas hushughulika na:

- Kutoa misaada ya dharura (chakula, maji, malazi) wakati wa majanga.
- Miradi ya maendeleo ya kijamii: kilimo, elimu, afya, maji safi, ujasiriamali.
- Kuelimisha jamii kuhusu haki, amani na utetezi wa mazingira.
- Kuhamasisha mshikamano wa kijamii, hasa kwa kuwajali maskini, wagonjwa, wazee, watoto yatima na wahamiaji.

Mfano; Ujenzi wa Visima vya maji vijijini, kuwasaidia wakulima kupata mbegu bora, Kutoa mafunzo ya ufundi kwa Vijana, kusaidia waathirika wa mafuriko n.k



Ufugaji wa kuku wa kienyeji na wa kisasa